TOLEO RAHISI LA

# ITIFAKI

## Uanzishaji wa Umoja wa Forodha wa Jumuia ya Afrika Mashariki

*Kwa msaada wa*

TRADE MARK EAST AFRICA

EASSI
Eastern African Sub-regional Support Initiative for the Advancement of Women

# *East Africa*



TOLEO RAHISI LA

# ITIFAKI

## Uanzishaji wa Umoja wa Forodha wa Jumuia ya Afrika Mashariki

Kampala, Uganda
2012

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Kuhusu EASSI | i |
| Dibaji | ii |
| 1.0 Utangulizi | 1 |
| 2.0 Umoja wa Forodha nini? | 1 |
| 3.0 Malengo ya Umoja wa Forodha ya Jumuia ya Afrika Mashariki ni yapi? | 2 |
| 4.0 Ni yapi Mawanda ya Umoja wa Forodha wa Jumuia ya Afrika Mashari-ki? | 2 |
| 5.0 Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Afrika mashariki ina sehemu zipi? | 2 |
| 6.0 Ni ya zipi sehemu za Itifaki ya Umoja wa Forodha yaJumuia ya Afrika Mashariki | 11 |
| 7.0 Ni ipi mipaka ya Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Jumuia ya Afrika Mashariki kwa mwanamke wa kawaida anayefanya biashara yake kati ya nchi za ukanda wa Afrika ya Afrika? | 12 |
| 8.0 Mapendekezo | 13 |
| 9.0 Hitimisho | 13 |
| 10.0 Viambatisho | 14 |
| Kiambatisho 1: Aina na vyanzo vya nyaraka zinazotumika kwenye EAC. | 15 |
| Kiambatisho 2: Hati Rahisi ya Uasili wa Bidhaa (SSCO) | 16 |

# Kuhusu EASSI

Asasi ya Mpango wa kuhamasisha maendeleo ya wanawake katika ukanda wa Mashariki mwa Afrika (EASSI) ni asasi ya kiraia ya kikanda iliyoanzishwa mwaka 1996. EASSI ina dhima ya kuwezesha ufuatiliaji wa utekelezaji wa makubaliano ya Jukwaa la Utendaji la Beijing (Beijing Platforms for Action [BPFAs]) ambacho ni chombo cha Mkutano wa nne wa wanawake uliofanyika mjini Beijing nchini China mwaka 1995. Asasi hii, ambayo imesajiliwa nchini Uganda kama asasi isiyo ya kibiashara, inafanya kazi na asasi nyingine za kitaifa katika nchi nne zikiwamo Burundi, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Somalia, Tanzania na Uganda.

## Dira yetu

Dira yetu ni kuwa na jamii yenye usawa wa kijinsia, yenye haki za kijamii, yenye amani na mendeleo.

## Dhima yetu

Dhima yetu ni kuhakikisha na kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Jukwaa la Utendaji la Beijing ili kuimarsha maendeleo ya wanawake na kupigania haki za kijamii.

## Malengo yetu

- Kusimamia maendeleo ya utekelezaji wa Jukwaa la Utendaji katika ukanda, kama njia ya kuziwajibisha serikali ili zitekeleze kwa vitendo ahadi zilizowekwa Beijing
- Kupigania kuwepo kwa chombo imara cha kikanda kinachopigania kuwepo kwa haki za wanawake na usawa wa kijinsia.
- Kuhimiza matumizi na mgawo mzuri wa raslimali za Umma, na matumizi haki za afya ya uzazi na jinsia na bajeti inayojali tofauti za kijinsia.
- Kuongeza ushiriki wa wanawake katika kutoa changamoto za kupinga vyanzo vya migogoro vya kimfumo kwa kutoa njia mbadala ya kujenga amani na kuleta suluhu ya migogoro.

## Utambulisho wetu wa kipekee

**Utambulisho wetu wa kipekee upo kwenye;**

- Uwanachama na mtandao wa kikanda ;
- Usimamizi wa utekelezaji wa Majukwaa ya Utendaji ya Afrika na Beijing ndani ya ukanda wa Mashariki mwa Afrika;
- Mlengo wetu wa Kiafrika wa kupigania haki za wanawake;
- Kuwa katika nafasi nzuri ya kusema kuhusu mwendelezo wa mapambano ya kupigania usawa wa kijinsia ndani ya ukanda wa Mashariki mwa Afrika kwa kutumia muundo wa Jukwaa la Utendaji;
- Wanachama tofauti wa watu binafsi na ule wa asasi wakiwa na uzoefu na uwezo tofauti wa kimaarifa kitaifa, kikanda na kimataifa.

# Dibaji

Asasi ya Mpango wa Kuhamasisha Maendeleo ya Wanawake katika Ukanda wa Mashariki mwa Afrika (EASSI) ni Asasi ya Kiraia ya Kikanda inayoundwa na watu binafsi waliojitoa, mashirika yasiyo ya kiserikali, miungano ya kimkakati na mitandao yenye nia ya kufanya mabadiliko ya mahusiano ya kijinsia ulimwenguni na hasa katika ukanda wa Mashariki mwa Afrika. Kazi yetu inafuata na kuzingatia makubaliano makubwa ya kimataifa ya Jukwaa la Utendaji la Beijing (BPFA) yanayotokana na Mkutano wa nne wa wanawake uliofanyika Beijing mwaka 1995. Maono ya makubaliano hayo yanathibitisha Mkataba wa Kukomesha aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW), na Mswaada kuhusu haki za wanawake. Kwa upande mwingine, BPFA imethibitishwa na tamko la pamoja na Malengo nane ya milenia (MDG) ya mwaka 2015 ambayo ni kupambana na umaskini, njaa, maradhi, kutojua kusoma na kuandika, na unyanyasaji wa kijinsia, pamoja na kujenga ushirikiano wa kimaendeleo.

Mkataba wa Uundaji wa Jumuia ya Afrika Mashariki unalitaja Soko la Pamoja la Afrika Mashariki kama hatua ya pili ambayo ingesaidia kuimarisha mshikamano wa kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiteknolojia, na katika Nyanja zingine. Soko hili litasaidia katika kuweka uwiano mzuri na endelevu kwa Nchi Wanachama. Pamoja na hayo Mkataba unatambua umuhimu wa wanawake na unapendekeza kuwa ushiriki wa wanawake uongezwe katika nyanja za biashara katika ngazi za uundaji na utekelezaji wa sera, uhamasishaji wa program maalumu kwa wanawake katika biashara ndogondogo, za kati na miradi mikubwa, uondoaji wa sheria, taratibu, na vitendo vyote vinavyofanya wanawake wasiweze kupata misaada ya kifedha ikiwa ni pamoja na mikopo na kutambulika na kutoa misaada kwa vikundi vya wanawake vya kitaifa na kikanda ambavyo vimeundwa kusaidia na kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika biashara na shughuli za kimaendeleo za kijamii. Ushirikiano huu wa kikanda unaundwa na watu wenyewe na unaongozwa na soko (katika sekta binafsi).

Toleo hili rahisi la Itifaki linatoa kwa ufupi mambo yaliyomo katika Itifaki katika mtindo unaoeleweka zaidi kwa wasomaji ili uwe rahisi kwa wanawake na waweze kuelewa. Toleo hili pia linatoa mwangaza waupenyo wa fursa kwa wanawake wafanyabiashara na linatoa mapendekezo kwa serikali na wadau wengine.

## 1.0 Utangulizi

Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Jamhuri ya Burundi, Jamhuri ya Rwanda, Jamhuri ya Kenya na Jamhuri ya Uganda ni Wadau wa Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuia ya Afrika Mashariki. Mkataba wa Uundwaji wa Jumuia ya Afrika Mashariki (1999) unasisitiza kuwepo kwa Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki ikiwa ndio msingi wa kujiimarisha kiuchumi, kijamii, kisiasa kiteknolojia na katika nyanja zingine ili kuweka uwiano mzuri kimaendeleo na kuleta maendeleo endelevu kwa Nchi Wanachama (Ibara za 75 & 151). Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki ilitiwa saini tarehe 2 Machi 2004 na ilianza kufanya kazi tarehe 1 Januari 2005.

Katika Ibara za 121 na 122, Mkataba wa uundwaji wa Jumuia ya Afrika Mashariki, unatambua umuhimu wa wanawake na unasisitiza uongezaji wa ushiriki wa wanawake katika biashara hasa katika ngazi za uundaji na utekelezaji wa sera, uhamasishaji wa program maalumu kwa wanawake wafanya biashara ndogondogo, za kati na wenye miradi mikubwa; uondoaji wa sheria, taratibu na mazoea vinavyozuia wanawake wasiweze kupata misaada ya kifedha ikiwa ni pamoja na mikopo, kutambulika na pamoja na kusaidiwa na vyama vya kibiashara vya wanawake kitaifa na kikanda ambavyo vimeundwa kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika biashara na shughuli za maendeleo ya Jumuia ya Afrika Mashariki. Ushirikiano huu wa kikanda unategemea na unatakiwa uwalenge watu na uendeshwe na watu wenyewe hasa sekta binafsi. Hii ina maana kuwa mahitaji ya wanawake nay ale ya Asasi za Kiraia yanazingatiwa.

## 2.0 Umoja wa Forodha ni nini?

Umoja wa Forodha ni kitendo cha kundi la nchi kukubaliana kuondoa viwango vya ndani vya ushuru na vizuizi vingine kwa bidhaa zinazozalishwa miongoni mwa Nchi Wanachama na, kwa pamoja, kuweka viwango vya ushuru mmoja kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka maeneo mengine duniani. Ushuru wa kuingiza bidhaa hautozwi miongoni mwa Nchi Wanachama ikiwa ni pamoja na kuondolewa kwa vizuizi vya kibiashara na uwekaji wa kiwango kimoja cha ushuru kwa bidhaa zinazotoka nje ya ukanda wa makubaliano.

Matokeo ya Umoja wa Forodha ni kuwa na bidhaa zinazozunguka ndani ya eneo husika na zinazolindwa zisiingiliwe na bidhaa kutoka maeneo mengine duniani.

## 3.0 Malengo ya Umoja wa Forodha wa Jumuia ya Afrika Mashariki ni yapi?

**Ibara ya 3** ya Itifaki inaonyesha kuwa lengo la Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Jumuia ya Afrika Mashariki ni kufungua biashara; kuhamasisha uzalishaji bora wa bidhaa; kuongeza uwekezaji wa bidhaa za ndani na za nje; kuhamasisha maendeleo ya kiuchumi na uzalishaji wa bidhaa tofauti tofauti ili kuongeza faida kwa Nchi Wanachama.

## 4.0 Ni yapi Mawanda ya Umoja wa Forodha wa Jumuia ya Afrika Mashariki?

**Ibara ya 4** inaonyesha kuwa mawanda ya Umoja wa Forodha wa Jumuia ya Afrika Mashariki yanajumuisha shughuli zinazofanywa pamoja miongoni mwa Nchi Wanachama katika nyanja za uendeshaji wa shughuli za forodha na kuweka uhuru wa biashara. Nyanja hizo ni pamoja na: kuwianisha na kurahisiha kanuni za forodha, taratibu na utunzaji wa nyaraka, kuhamasisha wa kuuzaji bidhaa nje na usimamiaji haki.

**5.0 Ni zipi sehemu za Itifaki ya Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki?** Itifaki ya Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ina sehemu nyingi kama zifuatazo:

### Sehemu A: Tafsiri

**Ibara ya 1** inatoa maana ya msamiati uliotumika kwenye Itifaki. Itifaki inatoa fasili ya msamiati muhimu wa kibiashara kama: ushuru wa pamoja wa Forodha, ushuru wa kijamii, upunguzaji wa athari za ruzuku; Ukanda Forodha, uhalifu wa forodha na vikwazo visivyo vya kiushuru.

### Sehemu B: Kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha wa Jumuia ya Afrika Mashariki

Ibara ya 1 na Ibara ya 2 inaonyesha kuwa ili kuhamasisha utekelezaji wa malengo ya Jumuiya yaliyoainishwa katika Ibara ya 5 ya Mkataba na kulingana na masharti ya Itifaki, Nchi Wanachama zitaunda Umoja wa Forodha ikiwa ni sehemu mojawapo ya sehemu za Jumuiya.

**Ibara ya 3** ya Itifaki inataja kuwa mojawapo ya malengo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kuweka huru biashara ndani ya ukanda kwa utaratibu wa kutafuta kufaidiana miongoni mwa wanachama; kuhamasisha uzalishaji bora ndani ya Jumuiya, kuimarisha biashara za ndani ; biashara ya mipakani na uwekezaji toka nje ndani ya Jumuiya na kukuza maendeleo ya kiuchumi na uzalishaji wa bidhaa tofauti tofauti ndani ya Jumuiya.

**Ibara ya 4** ya Itifaki ilivyo kwa shuguuli zingine zote za ushuru zinazofanywa na Nchi Wanachama katika kuendesha mambo ya forodha na biashara. Itifaki ya Umoja wa Forodha inatenda kazi kwa kanuni ya usawa, uondoaji wa ushuru wa ndani, uondoaji wa vikwazo visivyo vya kiushuru , uanzishwaji wa ushuru wa pamoja wa Forodha kwa bidhaa za nje, sheria za mahali itokapo bidhaa, sheria dhidi ya bidhaa zisizo na ubora (dumping), ruzuku na uwekaji wa kodi na kuweka uwiano kwa bidhaa zenye ruzuku, usalama pia usimamizi wa biashara, ushindani, urejeshaji wa malipo ya kodi (duty drawback), malipo ya malimbikizo, mabaki ya kodi na ushuru, ushirikiano wa forodha, usafirishaji upya wa bidhaa kwenda nje, urahisishaji na uwianishaji wa utunzaji wa nyaraka na taratibu, mifumo ya misamaha ya kodi, kuwianisha majina ya bidhaa na utoaji nembo na mwisho kuwa na bandari huru zisizokuwa na malipo.

**Sehemu ya C: Usimamizi wa forodha**

Inaelekeza mawanda ya ushirikiano katika Umoja wa Forodha kama

**Idara 5** inaonyesha kuwaNchi Wanachama watabadilishana taarifa kwa mambo yanayohusu forodha na biashara. Mambo hayo ni kama: kuzuia, kupeleleza na kupunguza uhalifu wa forodhani ; na hatua za kuwianisha mfumo wa taarifa ili kurahisisha ushirikiano wa mambo ya forodha na biashara. Hii inamaanisha kuwepo kwa ushirikiano baina Nchi Wanachama kwa kubadilishana taarifa, programu za pamoja, mikutano ya pamoja ya wataalamu wa mamlaka za mapato, Makamishina wakuu ili kuimarisha utendaji kazi wa mamlaka za mapato za katika ukanda huu. Inafanyika hivyo ili kuzuia, kupeleleza, kudhibiti mianya ya uhalifu bandarini. Na kuhakikisha kuwa mifumo ya taarifa inaoanishwa ili kurahisisha ushirikishanaji wa taarifa za forodha na biashara.

**Ibara ya 6** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama zinatakiwa kuanzisha urahisishaji wa biashara kwa kupunguza idadi ya nyaraka zinazohitajika katika biashara baina ya Nchi Wanachama, kutumia viwango vya aina moja vya nyaraka na taratibu za biashara na kutumia taratibu zinazofanana, kuhakikisha kuwepo kwa uratibu na upashanaji habari na mafunzo ya biashara ndani ya Jumuia.

**Ibara ya 7** inasema kwamba Nchi Wanachama zilikubaliana kurahisisha na kuoanisha nyaraka za forodha kufuata viwango vya kimataifa vya forodha ili kurahisisha ubadilishanaji wa bidhaa nadani ya Jumuia na kuhakikisha kwa uundwaji wa benki ya data za forodha kwenye sekretarieti.

**Ibara ya 8** Inaonyesha kuwa Nchi Wanachama zimekubali kupatanisha upangaji wa madaraja katika forodha na kurekebisha takwimu za biashara ya nje.

**Ibara ya 9** inasema kuwa Nchi Wanachama wamekubaliana kushirikiana katika kuzuia, kupeleleza na kudhibiti uhalifu wa forodha ndani ya mipaka yao na kuwasiliana baina yao kuhusu namna ya kuweka vituo vya pamoja vya mipakani.

**Ibara 10** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama wamekubaliana kufuta ushuru wote wa ndani na malipo mengine ambayo yanaweza kuathiri biashara.

**Ibara 11** inaonyesha kuwa Uundwaji wa Umoja wa Forodha utakuwa unaendela ndani ya kipindi cha miaka mitano ya mpito hadi Itifaki hii itakapoanza kutekelezwa.

**Ibara ya 12** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama zilikubaliana kuunda na kupitia upya viwango vya Ushuru wa pamoja kwa bidhaa za kutoka nje katika ngazi tatu: kiwango cha chini asilimia 0, cha kati kwa asilimia 10 kiwango cha juu cha asilimia 25 kwa bidhaa inayoingizwa kwenye Jumuia

**Ibara ya 13**, inaonyesha kuwa Nchi Wanachama zilikubaliana kuondoa Vizuizi Visivyokuwa vya Kiushuru (NTBs) kwa bidhaa zinazoingizwa ndani ya Nchi Wanachama. Waliunda njia inayoweza kutambua na kusimamia uondoaji wa vizuizi visivyokuwa vya kiushuru kama sheria, taratibu, utawala, na utaalamu unaohitajika nje ya ushuru ambao umewekwa na Nchi Mwanachama na ambao unaathari mbaya kwa biashara lazima uondolewe. Vizuizi vingi (NTBs) vinahusisha shughuli za forodha, na taratibu za utawala, matakwa kwa ajili ya ukaguzi, vizuizi vya barabarani, njia mbalimbali zinazoudhi na zenye kuleta gharama za matakwa ya ukaguzi na taratibu za kuvuka mipaka. Kuondolewa kwa hivi vizuizi kutawezesha kupungua kwa gharama kufanya biashara, kutafupisha taratibu za kupitisha mizigo mipakani na kutawezesha uwekezaji kati ya Nchi Wanachama.

**Ibara ya 14** inasema kuwa bidhaa zitakubalika wa taratibu za ushuru kama zimetokea ndani ya Nchi Mwanachama. Asili ya bidhaa itapimwa na kudhibitiwa na sheria ya udhibiti wa mahali bidhaa inapotoka ya Jumuia ya Afrika Mashariki, angalia kiambatisho III cha Itifaki.

**Ibara ya 15** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama hazitatengeneza sheria au kutumia njia zozote za kiutawala ambazo ni za kibaguzi kwa Nchi nyingine Mwanachama.

**Ibara ya 16** inaonyesha kuwa uingizaji wa bidhaa hafifu hauruhusiwi endapo zinaathiri viwanda vya Nchi yoyote Mwanachama, kulingana na sheria za Kuzuia Uuzaji wa bidhaa hafifu kama zilivyoainishwa kwenye Kiambatisho cha Itifaki.

**Ibara ya 17** inasema kuwa endapo Nchi Mwanachama itatoa au itaendeleza ruzuku ikiwa ni kwa njia ya mapato au ya kusaidia bei, ambayo inatumika moja kwa moja ama isiyo ya moja kwa moja, kuharibu ushindani kwa kupendelea bidhaa fulani au uzalishaji wa bidhaa fulani katika Nchi Mwanachama, itatoa taarifa ya maandishi kwa Nchi nyingine Mwanachama.

**Ibara ya 18** inaonyesha kuwa, ili kufidia athari za ruzuku, ambazo zinategemea urekebishaji wa soko, Nchi Wanachama zinaweza kuiwekea kodi bidhaa au kuweka kodi kuleta uwiano kwa bidhaa yenye ruzuku kutoka nchi iliyoingizwa.
Ibara ya 19 inasema kuwa Nchi Wanachama zimekubaliana kuchukua tahadhali iwapo kutaibuka bidhaa fulani kutoka nje ya soko inaiyoingia ndani ya soko la Nchi Wanachama.

**Ibara ya 20** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama zilikubaliana kushirikiana katika kugundua na kupeleleza uuzaji kwa bei nafuu biadha, na uingizaji wa ghafla wa bidhaa na ulazimishaji wa wa hatua zilizokubalika kupambana na mazoea hayo kwa kuwa yanafifisha ushindani.

**Ibara ya 21** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama zitapiga marufuku vitendo vyote vinavyoathiri soko huria ikiwa ni pamoja na makubaliano, maamuzi au maafikiano ambayo yana lengo au madhara ya kuzuia, kubana au kuharibu ushindani ndani ya Jumuia. Hili litafanyika kwa kuzingatia sheria na sera za Ushindani za Jumuia ya Afrika Mashariki.

**Ibara ya 22** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama baada ya kutoa taarifa kwa Katibu Mkuu kuhusu nia yao ya kuanzisha ua kuendelea kuweka vikwazo au vizuizi vianavyo athiri sheria za usalama na taratibu, uthibiti wa silaha, silaha za kivita, vifaa vya kijeshi, ulinzi na usalama wa maisha ya watu, mazingira na hifadhi asilia, afya ya jamii, au maadili ya jamii na utunzaji na usalama wa wanyama pori.

**Ibara ya 23** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama watachukua hatua kuhakikisha kuwa bidhaa zinazosafirishwa kwa mara nyingine zitasamehewa ushuru wa kuingia au kutoka, hata hivyo hii haihusishi kodi ya utawala na gharama za huduma kwa kuingiza au kutoa bidhaa ya aina hiyo kulingana na sheria za nchi na taratibu wan chi wanachama.

**Ibara ya 24** inaunda kamati ya kufuatilia biashara ya Jumuia ya Afrika Mashariki ambayo itakuwa na kazi ya kushughulikia masuala ya sheria ya asili ya bidhaa, hatua dhidi upunguzaji bei kwa bidhaa hafifu, ruzuku na utozadi kodi kufidia ruzuku ili kweka usawa wa bei, hatua za kiusalama, na kusuluhisha migogoro.

**Sehemu D: Kuweka Biashara huria**

**Ibara ya 25** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama zimekubaliana kusaidia jamii katika kukuzaji wa miradi ya uuzaji bidhaa nje ya nchi ili kuharakisha maendeleo, kuhamasisha na kurahisisha uwekezaji katika miradi inayojikita kwenye malengo ya usafirishaji nje, kuzalisha bidhaa zilizo na kiwango cha kimataifa cha ushindani, kutengeneza mazingira ya miradi ya kukuza usafirishaji bidhaa nje na kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje. Uuzaji wa bidhaa katika eneo la forodha utapewa ruhusa na mamlaka yenye dhamana hiyo.

**Ibara 26 i**naonyesha kuwa inapotokea kusafirisha bidhaa kwenda nje, urudishaji wa ushuru uliolipwa kimakosa unaweza kuruhusuwa kwa kiwango fulani na kwa masharti ambayo yatatolewa na mamlaka yenye dhamana hiyo. Haya yote yatafanywa kwa kufuata mipango ya urejeshaji wa ushuru uliotolewa kimakosa kama iliyokubaliwa na sheria ya forodha ya Jumuia.

**Ibara ya 27** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama zitasaidia kuhamasisha uuzaji wa bidhaa nje kwa kuweka punguzo kwenye ushuru na kodi ya ongezeko la thamani.

**Ibara ya 28** inasema kuwa Nchi Wanachama zitasaidia kukuzauuzaji wa bidhaa nje kwa kurahisisha utengenezaji wa bidhaa kwa kutumia mifumo ya dhamana iliyopo katika nchi husika. Utaaratibu wa uzalishaji wa bidhaa chini ya dhamana utaruhusu bidhaa kutoka nje kutumika ndani ya eneo la forodha kwa ajili ya usindikaji na uzalishaji wa bidhaa.

**Ibara ya 29** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama zimekubali kusaidia uanzishwaji maeneo maalumu ya kiuchumi (EPZ). Uingiaji kwenye EPZ utasababisha punguzo la malipo ya ushuru kwa bidhaa zinazoingia toka nje, na ambazo zinatumika moja kwa moja katika uzalishaji wa bidhaa za kuuza nje ambapo uuzaji huo utafanywa na mtu mwenye kibali cha kufanya kazi hiyo ndani ya ukanda huo.

**Ibara ya 30** inasema kuwa Baraza linaweza mara kwa mara kukubali na kupitisha uundwaji wa mifumo mingine ya kukuza uuzaji wa bidhaa nje kadiri itakavyolazimu.

**Sehemu E: Mambo Yanayohusu Biashara Masuala yanayohusu biashara ni yale yanayosaidia na kudumisha shuguli za kibiashara.**

Mambo hayo yanajumuisha: matakwa ya bidhaa kufikia viwango vya kisheria kwenye nchi inakotoka na kufutwa kwa kwa vizuizi visivyokuwa vya kiushuru miongoni mwa Nchi Wanachama. Mambo haya yanafuta sheria ya kibaguzi kwa bidhaa zinazofanana zinazotoka miongoni mwa Nchi Wanachama. Pia yanafuta uwezekano wa kuingiza bidhaa hafifu. Mambo haya pia yanalazimisha kutolewa kwa Nchi Wanachama endapo nchi moja itatoa ruzuku kwa bidhaa na hivyo kuharibu ushindani, ili kuchukua hatua ntingine za kuleta uwiano kwa kupunguza athari za ruzuku hiyo.

Mambo hayo pia yanatoa namna ya kulinda wazalishaji wa ndani kutokana na uingizaji ul-iokithiri wa bidhaa toka nje. Kwa hiyo, Nchi Wanachama zinatakiwa kushirikiana kupam-bana na tatizo hilo. Kufanya hivyo kunawezesha mzunguko wa bidhaa na huduma na waka-ti huo huo kukiwa na mwanya kwa Nchi Wanachama kuweka vizuizi vya kibiashara kwa bidhaa nyeti kama  silaha kwa kuweka ushuru wa pamoja. Mambo haya pia yanawezesha uanzishaji wa Kamati ya EAC ya Usuluhishi wa Migogoro ya Kibiashara, ili kutoa maamuzi kwa migogoro ya kibiasharandani ya eneo la Jumuia ya Afrika Mashariki.

**Ibara ya 14** Sheria ya uasili – Bidhaa itakubalika kuingia kwenye ukanda wa pamoja wa ushuru bidhaa hiyo imezalishwa miongoni mwa Nchi Wanachama na na inakidhi vigezo vya kisheria vya Uasili (Kiambatisho cha III).

**Ibara ya 15**: Wadau wanaoshughulikia maswala ya kodi katika ngazi ya taifa hawataweka sheria au kutumia mbinu za kiutawala ambazo zinabagua bidhaa za aina moja kutoka nchi nyingine mwanachama au kwa kuweka kodi ili kuzilinda bidhaa jingine.

**Ibara ya 16**: Sheria Dhidi ya Uingizaji wa Bidhaa Hafifu (Anti-dumping Measures)- Nchi Wanachama zinatambua kuwa uingizaji kwa wingi bidhaa hafifu hauruhusiwi endapo ni hatari kwa bidhaa za kiwanda kilichomo Nchi Mwanachama. Ikitokea kuwepo kwa bidhaa kama hizo, Katibu Mkuu wa EAC atalijulisha shirika la Biashara Duniani (WTO) kuhusiana na hatua za kuzuia uuzaji huu wa hila zinazochukuliwa na Nchi Wanachama. (Kiambatisho IV cha Itifaki hii).

**Ibara ya 17:** Ruzuku-Ikiwa Nchi Mwanachama itatoa au kubakiza ruzuku, aina yoyote ile iwe ni ya kimapato au ya kusaidia bei imbayo nchi hiyo inainatumia kuharibu ushindani, na kutoa upendeleo fulani kwa bidhaa au uzalishaji wa bidhaa fulani. Nchi mwathirika wa ruzuku hii itatoa taarifa kwa nchi zingine kwa maandishi.

**Ibara ya 18:** Kodi ya kuleta usawa (contrevailing measures) – Jumuia ya Afrika Mashariki inaweza, kwa lengo la kuweka uwiano sawa wa ruzuku na kulingana na sheria, ikatoza ushu-ru wa kusawazisha kwa bidhaa yoyote kutoka nje inayoingizwa kwenye Umoja wa Forodha ambayo imewekewa ushuru unaoathiri ushindani (Kiambatisho V cha Itifaki).

**Ibara ya 19** Hatua za Tahadhari – Nchi Wanachama zimekubalina kuchukua hatua za tahadhari ikitokea kuna uingiaji wa ghafla wa bidhaa ndani ya Nchi Mwanachama. Hali hiyo inaweza kutishia au kuathiri wazalishaji wa ndani au bidhaa zilizoko kwenye ushinda-ni ndani ya nchi husika. Hili linatakiwa kufanywa ndani ya miaka mitano ya mpito ya matumizi ya Itifaki ya Umoja wa Forodha na kulingana na sheria ya Umoja wa Forodha wa Jumuia ya Afrika Mashariki (kiambatisho VI)

**Ibara ya 20**: Ushirikiano – Nchi Wanachama zimekubaliana kushirikiana katika kugundua, kupeleleza matukio yote ya: uingizaji kwa wingi wa bidhaa za bei nafuu; uwekaji usiorasmi wa ruzuku, na uingiaji wa ghafla wa bidhaa, na zinaweza kuchukua hatua za kudhibiti haya. Endapo kuna ushahidi wowote wa bidhaa kuingia kwa ghafla, kuuzwa kwa bei ya hila, au uuzaji wa bidhaa iliyona ruzuku kutoka nchi ya kigeni ndani ya soko la Umoja wa Forodha, nchi iliyoathirika inaweza kuiomba nchi ambamo bidhaa hiyo inaingizwa kuweka masharti ya tahadhari. Ikiwa nchi iliyoombwa haitachukua hatua ndani ya siku 30 kutoka siku iliyotaarifiwa, nchi inayolalamika itatoa taarifa kwa mamlaka husika ndani ya Umoja wa Forodha ambako itabidi hatua ichukuliwe

**Ibara ya 21:** Ushindani -Nchi Wanachama zitazuia kitendo chochote ambacho kinaathiri uhuru za biashara ikiwa ni pamoja na makubaliano, mipango au utekelezaji wa dhati ambao una malengo au una athari ya kuzuia au kubana uwanja wa ushindani ndani ya Jumuia. Hii itafanywa chini ya sera na sheria ya Ushindani ya Jumuia ya Afrika Mashariki.

**Ibara ya 22:** Mikakati ya kudhibiti na Kuzuia Biashara – Nchi Mwanachama inaweza, baada ya kutoa taarifa kwa Katibu Mkuu, kueleza nia yake ya kuanzisha au kuendelea kutumia njia za kudhibiti au kuzuia biashara ambazo zinaweza kuathiri vifuatavyo: matumizi ya sheria ya usalama, udhibiti wa silaha na vifaa vingine au bidhaa za kijeshi, kulinda maisha ya watu, mazingira, mali asili, usalama wa umma, maadili ya umma na kulinda wanyama na mimea. Hata hivyo, Nchi Mwanachama haitaitumia haki hiyo kwa lengo la kudhibiti mzunguko huru wa bidhaa zingine ndani ya Jumuia ya Afrika Mashariki. Nchi Wanachama zilikubaliana kutaja bidhaa ambazo zitakuwa zinathibitiwa na zile zisizoruhusiwa katika soko.

**Ibara ya 23**: Uuzaji Bidhaa nje kwa Mara ya Pili- Nchi Wanachama zitahakikisha kuwa bidhaa inayouzwa nje kwa mara ya pili haitozwi ushuru wa kuingilia au kutokea nchi moja kwenda nyingine kulingana na sheria ya Forodha ya Jumuia. Hata hivyo, hii haimaanishi kuacha kutoza gharama za kiutawala na huduma zinazotolewa katika kuingiza au kutoa ndani ya nchi kwa bidhaa za aina hiyo kulingana na taratibu na sheria za kitaifa na kanuni za Nchi Wanachama.

**Ibara ya 24**: Kamati ya EAC ya Usuluhishi wa Kibiashara-Kamati itaundwa na wajumbe tisa ambao ni watu wenye ujuzi na waliobobea katika masuala ya biashara, ushuru wa forodha na sheria. Kila Nchi Mwanachama itawachagua wajumbe watatu kuingia kwenye Kamati. Kamati hii itakuwa na kazi nyingi ambazo zimetajwa kwenye Itifaki, miongoni mwazo ni: kuchunguza migogoro, kuthibitisha kutokea kwa migogoro, kutoa mapendekezo na kutoa taarifa kwenye Baraza la mawaziri la EAC kuhusu masuala waliyoyashughulikia na maamuzi yaliyotolewa. Maamuzi ya kamati kuhusiana na usuluhishaji wa migogoro ni ya mwisho, isipokuwa kama maamuzi hayo yako chini ya Kanuni za Umoja wa Forodha wa Jumuia ya Afrika Mashariki.

**Sehemu F: Mirpango ya Uhamasishajii wa Biashara**

Mipango ya Uhamasishaji wa biashara ni usaidizi unatolewa na Nchi Wanachama kuhakikisha uzalishaji wa wa bidhaa zenye ushindani kwa ajili ya biashara ya nje kwa safari za kibiashara, maonyesho ya kibiashara, au mipango ya utafutaji wa masoko. Mipango hii inaruhusu msamaha wa kodi kila inapotakiwa, na punguzo ushuru na VAT ikiwa ni pamoja na uundwaji wa Kanda maalumu za kiuchumi (EPZ) ndani ya Jumuia ya Afrika Mashariki.

**Ibara ya 25:** Inasema kuwa Nchi Wanachama wamekubali kuhamasisha uuzaji bidha nje ya Jumuia ili kuongeza maendeleo, kukuza na kuhakikisha kuwa bidhaa zinazozalishwa zina ubora ili kuvutia wawekezaji wa nje. Bidhaa hizo zinapokuwa zimeuzwa kwenye eneo la ushuru la Jumuia ya Afrika Mashariki zitavutia na kuongeza kodi na malipo kwenye ushuru wa pamoja wa Forodha.

**Ibara ya 26** inasema kuwa pale ambapo misamaha ya kodi inaweza kuruhusiwa kama kwenye bidhaa au na vifaa vya kuchakatia au kusindikia bidhaa viwandani zilizo chini ya sheria za Forodha za Jumuia.

**Ibara ya 27** inaeleza mipango ya punguzo la ushuru na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ili kuimarisha mipango ya kuongeza uuzaji bidhaa nje kama inavyoelezwa kwenye sheria za forodha za Jumuia ya Afrika Mashariki.

**Ibara ya 28** Nchi Wanachama zimekubaliana kuuunga mkono juhudi za kukuza uzalishaji kwa ajili ya kuuza nje kwa kukopesha ili kusaidia ndani ya nchi kulingana na sheria za Forodha. Taratibu hizi za kukopesha na kutoa dhamana za usindikaji unaruhusu bidhaa zilizoingizwa kutumika kwenye eneo la Umoja wa Forodha kwa ajili ya kuchakata au kusindika. Ushuru na kodi zitalipwa kwa njia ya kufidia bidhaa.

**Ibara ya 29**: Nchi Wanachama zilikubaliana kusaidia uundwaji Kanda maalumu za kiuchumi kulingana na sheria ya Umoja wa Forodha wa Jumuia ya Afrika Mashariki na kanuni zilizobainishwa kwenye kiambatisho VII cha Itifaki.

**Sehemu G: Kanda Maalumu za Kiuchumi**

Ibara ya 31 inasema kuwa Nchi Wanachama zinaweza kuamua kuuunda bandari huru kwa lengo la kuwezesha na kukuza biashara za kimataifa, na kuharakisha maendeleo ndani ya Umoja wa Forodha, ili kukuza na kuhamasisha biashara ya bidhaa zilizoingizwa kupitia bandari huru. Bidhaa inayoingia katika bandari huru itasemehewa ushuru wa forodha na kodi zingine isipokuwa pale ambapo bidhaa inaondolewa kutoka badanri huru kwenda kutumika majumbani.

**Ibara ya 32** inaonyesha kuwa Baraza linaweza kupitisha uanzishwaji wa mipango mingine maalumu ya kiuchumi kwa lengo la kuimarisha uchumi wa Nchi Wanachama. Bandari huru zinaweza kuwa maeneo ya Bandari za bahari au mito, viwanja vya ndege, au maeneo megine yenye faida hizo hizo za kijiografia na kiuchumi.

**Sehemu H: Mifumo ya Misamaha ya kodi**

**Ibara ya 33** inasema kuwa Nchi Wanachama zimekubali kuoanisha mifumo yao ya misamaha ya kodi na kutumia orodha ya bidhaa zilizoafikiwa kupewa wa msamaha wa kodi; yaani bidhaa ambazo hazitozwi ushuru wa forodha.

**Ibara ya 34** inaonyesha kuwa uendeshaji wa Umoja wa Forodha ukijumuisha ni pamoja ule wa mambo ya sheria, utawala na mambo ya kitaasisi utatawaliwa na sheria ya Forodha ya Jumuia ya Afrika Mashariki.

**Ibara ya 35** inaonyesha kuwa, kwa ajili ya Itifaki hii, Baraza litapitisha hatua zitakazochukuliwa kutaja na kuonyesha tofauti zinazoweza kujitokeza kutokana na Uanzishaji wa Umoja wa Forodha.

**Ibara ya 36** inasema kuwa ikitokea kuathirika au hatari ya kuathirika kiuchumi katika nchi moja kutokana na matumizi ya Itifaki hii, Nchi Mwanachama italitaarifu Baraza kupitia kwa Katibu Mkuu na wanachama wengine watachukua hatua za kiusalama.

**Ibara ya 37** inaonyesha kuwa Nchi Wanachama zitaheshimu na kutimiza ahadi na maamuzi yao kulingana sheria na masharti ya mashirika mengine yakiwamo yale ya Kimataifa ambayo wao ni wajumbe.

**Ibara ya 38** inaonyesha kuwa matumizi ya Itifaki yatatambua masharti ya Mkataba kwenye maeneo mengine ya ushirikianao ikiwa ni pamoja na ushirikiano katika uendeshaji wa masuala ya mazingira na maliasili, viwango vya ubora, udhibiti wa ubora, vipimo na upimaji; usalama wa chakula na sheria za afya ya wanyama na mimea; haki za uvumbuzi; na viwango na taratibu za kiufundi.

**Ibara ya 39** inasema kuwa sheria ya Jumuiya ya mambo ya forodha itakuwa na vipengele vinavyotokana na Mkataba, Itifaki ya Umoja wa Forodha na viambatisho, kanuni na maelekezo yanayotolewa na Baraza, maamuzi ya mahakama yanayohusika, sheria za Jumuiya zilizopitishwa na Bunge la Jumuiya na kanuni za sheria za kimataifa.

**Ibara ya 40** inaonyesha kuwa, hatimaye Nchi Wanachama zimekubaliana kabla ya Itifaki kuanza kufanya kazi, kuwa viambatisho vilivyomo ndani ya Itifaki hii vitakuwa ni sehemu mojawapo ya Itifaki.

**Ibara ya 41** Inaonyesha kuwa Nchi Wanachama zimekubaliana kutii kanuni za kuthibiti na kutatua migogoro na kwamba zinatumia kanuni hizo kwa nia njema na maamuzi yoyote yakayotolewa na chombo cha Jumuiya kinachoshughulikia migogoro.

**Ibara ya 42 i**naonyesha kuwa Itifaki ya Umoja wa Forodha inaweza kurekebishwa na Nchi Wanachama kulingana na ibara ya 150 ya mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuia ya Afrika Mashariki.

**Ibara ya 43** inaonyesha kuwa Itifaki itaanza kutumika pale itakapoidhinishwa kwa barua rasmi itakayosainiwa na Nchi zote Wanachama pamoja na Katibu Mkuu.

**Ibara ya 44** inasema kuwa Itifaki na vyombo vyote vya uidhinishaji vitawasilishwa na Katibu Mkuu na ambaye atawasilisha pia nakala halisi za Itifaki na vyombo vya uinishaji kwa Nchi zote Wanachama. Katibu Mkuu anatakiwa kusaijili Itifaki kwenye Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa, Shirika la Biashara la Kimataifa, Shirika la Kimataifa la Forodha na mashirika mengine kadiri Baraza litakavyopendekeza.

## 6.0 Ni nini faida za Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Jumuia ya Afrika Mashariki kwa wanawake wanaofanya biashara mipakani?

- Wanawake wengi zaidi wanaweza kupita ofisi za Forodha kwa sababu ya uharaka wa kupitisha bidhaa na upatikanaji wa taarifa kuhusu masuala ya kodi;
- Kuongeza biashara za mipakani kwa wanawake ikiwa ni matokeo ya mzunguko rahisi na wa bure wa bidhaa mipakani;
- Kuongezeka kwa ushiriki wa wanawake katika biashara za mipakani;
- Kupunguza gharama za kufanya biashara, kufupisha muda wa utoaji wa mizigo na kuongeza faida;
- Kuna njia na mianya kwa wanawake kupitishia malalamiko kuhusiana na vizuizi au kukataliwa kufanya biashara naNchi Mwanachama;
- Wanawake wanapata fursa ya kubainisha na kushughulikia changamoto zinazowakabiri kupitia majukwaa ya kibiashara ya wanawake wakishirikiana na wakala wa serikali.

## 7.0 Ni ipi mipaka ya Itifaki ya Umoja wa Forodha ya Jumuia ya Afrika Mashariki kwa wanawake wanaojihusisha na Biashara za mipakani katika ukanda wa Afrika Mashariki?

**Mipaka inahusisha:**

1. Asilimia kubwa ya wanawake wanaojihusisha na Biashara za mipakani wana uelewa mdogo. Wanategemea sana watu wa kati kufanya biashara hizo na kupitisha bidhaa mipakanikwa niaba yao.
2. Ingawa kwa sasa utaratibu wa kuondoa mizigo bandarini umerahisishwa, wanawake wengi wafanya biashara wanatumia mawakala na hivyo kutumia gharama kubwa zisizo za lazima.
3. Wanawake wafanyabiashara wanakumbana na changamoto za kifedha ili kuansisha na kuendeleza biashara zao. Masharti katili ya mabenki, kuwa hayako tayari kutoa mikopo kwa watu wasio na dhamana au walio na dhamana ndogo ya mkopo, yanaleta ugumu kwa wanawake wengi wanafanya biashara ndogondogo kwa sababu wengi wao hawamiliki mali inayoweza kuwawezesha kuweka dhamana. Hata Taasisi ndogo za kifedha (Microfinance) zina masharti magumu ambayo wanawake wenye kipato kidogo hawawezi kuyatekeleza.
4. Hata kama wakiwa na bidhaa ndogo wanawake wafanya biashara ndogo ndogo hutumia njia za panya ambazo ni hatari na za gharama sana. Ni gharama kuwalipa wabebaji na wanaopitisha biashara kimagendo mipakani. Wakati mwingine wabebaji hao huiba bidhaa na kuziuza kwingine; hivyo husababisha hasara.
5. Ukosefu wa taarifa kuhusu biashara na masoko ya ndani na katika ukanda. Ingawa Umoja wa Forodha wa EAC umekuwapo kwa karibu miaka 12 sasa, wanawake wafanya biashara hawaujui.
6. Bidhaa zinazouzwa na kununuliwa ni za aina tofauti tofauti zikiwa ni pamoja na bidhaa za vyakula (nafaka, maharage, mbogamboga, matunda), vyombo vya ufundi, samani, vito, vifaa vya umeme, manukato, nk. Baadhi ya bidhaa zinatakiwa kuandaliwa ili ziwe salama kwa afya ya wanyama na mimea (SPS). Wanawake wengi hawana uwezo wa kufikia viwango vya chini kabisa vya masharti hayo.

## 8.0 Mapendekezo

1. Serikali inabidi zirahisishe sheria, sera na taratibu zote za biashara kwa faida ya wanawake;
2. Anahitajika wakala maalumu wa Serikali kuwafundisha wanawake wafanya biashara mbinu za kuboresha bidhaa zao na kusindika ili kufikia viwango vinavyotakiwa na soko.
3. Inabidi Serikali iingilie kati na kuyalazimisha mabenki na taasisi ndogondogo za kifedha kupunguza masharti kwa kutumia mfumo wa kuokoa hela halisi iliyokopeshwa badala ya mfumo wa masharti makali na ya kibaguzi ili wanawake wengi zaidi waweze kupata mikopo na kuanzisha au kuendeleza biashara.
4. Inabidi Serikali iunde na kusaidia taasisi zinazojishughulisha na wanawake wafanyabiashara ili kuboresha viwango vya na ufungaji wa bidhaa kukidhi viwango vya soko la ukanda huu;
5. Inabidi Serikali na iweke mifumo thabiti ya: kuratibu idadi ya wanawake wafanya biashara wanaovuka mipaka/wanaofanyakazi bila watu wa kati; tabia za maofisi wa mipakani kwa wanawake na kwa ujumla kuratibu mabadiliko ya ushiriki wa wanawake katika biashara za kuvuka mipaka;
6. Inabidi serikali itafsiri tarifa zilizomo ndani ya Itifaki ya Umoja wa Forodha ya Jumuia ya Afrika Mashariki kwenye lugha rahisi inayotumiwa na wanawake wafanya biashara. Ingawa ni muhimu kuhakikisha kuwa kuna kupashana habari ndani ya Itifaki ya Umoja wa Forodha ya Jumuia ya Afrika Mashariki, ni vizuri kuziweka taarifa hizo katika lugha rahisi ambayo inatumiwa na wanawake walio wengi ili waelewe na wafaidike na taarifa hizo.
7. Inabidi serikali ijihusishe na kuhamasisha wanawake kuhusu biashara za kuvuka mipaka ili kuwawezesha kutumia fursa na kufaidika na fursa zilizotajwa pamoja na kuwaandaa na changamoto mbalimbali na namna ya kukabiliana na changamoto hizo wakati wa utekelezaji wa Umoja wa Forodha wa Jumuia ya Afrika Mashariki.

## 9.0 Hitimisho

Itifaki ya Uundwaji wa Jumuia ya Afrika Mashariki inatoa fursa kwa wanawake wote na wanaweza kuzitumia fursa hizo kuboresha hali zao za kiuchumi. Hata hivyo, mambo mengi yanategemea, kwa kiwango kikubwa, ufuatiliaji wa pamoja na si utekelezaji wa mtu mmoja mmoja. Utekelezaji wa Umoja wa Forodha wa Jumuia ya Afrika Mashariki inabidi uhakikishe ushiriki wa wanaume na wanawake, sekta zote za kiuchumi na serikali, katika kuongeza idadi na ubora wa ushiriki.

# 10. VIAMBATISHO

## Kiambatisho 1: AINA NA VYANZO VYA NYARAKA ZINAZOTUMIKA KWENYE EAC

| Aina ya waraka | Nyaraka za muda za kusafiria | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Nchi | Uganda | Tanzania | Kenya | Rwanda | Burundi |
| Ada | UGX 5000 | TSH 10,000 | KSH 300 | Bure | N/A |
| Mahali | Ofisi za Uhamiaji katika mipaka yote ya Uganda | Ofisi za Uhamiaji Arusha na mipakani kote | Idara ya Uhamiaji Mipakani na Makao makuu ya Uhamiaji Nairobi | Ofisi za Uhamiaji katika mipaka yote | Ofisi za Uhamiaji katika mipaka yote |
| Aina ya waraka | Pasipoti ya EAC | | | | |
| Ada | UGX 52,000 | TSH 30,000 | KSH 940 | 20,000Rf | N/A |
| Mahali | Idara ya Uhamiaji makao makuu | Idara ya Uhamiaji Dar-es-saalam au Arusha | Idara ya Uhamiaji makao makuu Nai-robi, Nyayo House | Idara ya Uhamiaji makao makuu Ki-gali. | Paspoti ya Afrika Mashariki haijaanza kutumika nchini Burundi |
| Aina ya waraka | Pasipoti ka Kitaifa | | | | |
| Ada | UGX 82,000 | TSH 50,000 | KSH 3040 (for a 32 pages passport) | 50,000Rf | 135,000BF |
| Mahali | Idara ya uhamiajim katika ofisi za wilaya, Wizara ya Mabo ya ndani Idara ya pasipoti makao makuu | Ofisi za Uhamiaji Dar es Salaam | Ofisi za Uhamiaji Nyayo house | Mako makuu ya Uhamiaji Kigali | Mako makuu ya Uhamiaji Bujum-bura |



| Aina ya waraka | Nyaraka za muda za kusafiria | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Nchi | Uganda | Tanzania | Kenya | Rwanda | Burundi |
| Ada | UGX 5000 | TSH 10,000 | KSH 300 | Bure | N/A |
| Mahali | Ofisi za Uhamiaji katika mipaka yote ya Uganda | Ofisi za Uhamiaji Arusha na mipakani kote | Idara ya Uhamiaji Mipakani na Makao makuu ya Uhamiaji Nairobi | Ofisi za Uhamiaji katika mipaka yote | Ofisi za Uhamiaji katika mipaka yote |
| Aina ya waraka | Pasipoti ya EAC | | | | |
| Ada | UGX 52,000 | TSH 30,000 | KSH 940 | 20,000Rf | N/A |
| Mahali | Idara ya Uhamiaji makao makuu | Idara ya Uhamiaji Dar-es-saalam au Arusha | Idara ya Uhamiaji makao makuu Nai-robi, Nyayo House | Idara ya Uhamiaji makao makuu Ki-gali. | Paspoti ya Afrika Mashariki haijaanza kutumika nchini Burundi |



**ANGALIZO: Kuna hati za nyongeza kwa bidhaa maalumu**

Kwa biashara ya wanyama, unatakiwa kuwa na kibali cha kusafirisha wanyama na biadha za wanyama na Cheti cha Afya ya Wanyama

Kwa mbwa na paka unatakiwa na kibali cha kusafirisha mbwa na paka

(Nyaraka hizi zinaweza kupatikana katika idara ya mifugo na entomolojia – Wizara ya Mifugo na Uvuvi)

**Nyingine**

Kwa vyakula na vinywaji, ni lazima uwe na cheti cha uchambuzi kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali

Kwa samaki, unatakiwa kuwa na kibali cha kusafirisha samaki na Cheti cha Afya kutoka idara ya uvuvi – Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

# KIAMBATISHO 2: HATI RAHISI YA UASILI WA BIDHAA (SSCO)



EAST AFRICAN COMMUNITY
SIMPLIFIED CERTIFICATE OF ORIGIN
(For goods of a value not exceeding US $ 500)
*(Kwa bidhaa zenye thamani isiyozidi US$ 500)*

1) Exporter (name, full address, country)
*Msafirishaji (Jina na anwani)*

Reference Number ...............
*Kumb Na*

2) Importer (Names & address)
*Mwingizaji bidhaa, ( Jina na anwani yake)*

3)Country of Origin
*Uthibitisho wa uasili wa bidhaa*

4)Description of goods
*Maelezo ya bidhaa*

5)No. and type of packages
*Namba na aina ya kifurushi*

6)Value
*Thamani*

7)Declaration by Exporter
*Tamko la Msafirishaji/Mzalishaji/Mgavi*

I, the undersigned
Mr/Mrs/Ms.............................. declare that the goods described above have been produced (country).......................in accordance with the EAC Rules of Origin.

Signature..........................................
*(Saini)*
Place................................................
*(Mahali)*
Date.................................................
*(Tarehe)*
Official stamp
*(Mhuri)*

8)Customs Endorsement
*Uthibitisho wa forodha*
I, the undersigned, hereby endorse the exporters' declaration and certify that the goods qualify under the EAC Rules of Origin.

Signature..........................................
*(Saini)*
Place................................................
*(Mahali)*
Date.................................................
*(Tarehe)*
Official stamp
*(Mhuri)*

© EASSI 2012

Haki zote zimehifadhiwa. Kuchapisha tena kitabu chote au sehemu kwa madhumuni ya kueleimisha au yasiyo ya kibiashara kunaruhusiwa lakini baada ya ruhusa ya maandishi kutoka kwa mwenye dhamana ya haki miliki iwapo tu mtumiaji ataonyesha kwa uwazi chanzo na nyongeza au badadilisho yoyote, kama yatakayokuwepo.

*The Eastern African Sub-regional Support Initiative for the Advancement of Women (EASSI), P.O.Box 24965, Kampala, Uganda,*
*Tel: +256414285163/312 266 451*